TANGAZO LA SERIKALI Na. 670 La Tarehe. 21/8/2020

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA. 290

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA ZA MWAKA 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya Sengerema za Mwaka 2020.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema;

Sura ya 287

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni kifusi, udongo, mchanga, tarazo, moramu, mawe, kokoto, mawe, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema au afisa

yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada na ushuru

3.- (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

4. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwari la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

5.- (1) Muda wa kukusanya ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum

kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada na ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

6.- (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo utakuwa

umesababishwa na Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

7.- (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

8. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa nia ya kukusanya ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa na adhabu

9.- (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii; au

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri shughuli

zinazohitaji kulipiwa ushuru.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha kwanza atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne.

Kufifilisha kosa

10.- Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Tangazo la Serikali na. 440/2013

11.- Sheria Ndogo hizi zinafuta Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema (Ada na Ushuru) za mwaka 2013.

*Tangazo la Serikali Na. 670 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

*(Chini ya Kifungu cha 4)*

| 1.USHURU WA MADINI NA UJENZI | | |
|---|---|---|
| *Na.* | *Aina ya Madini* | *Kiwango cha Ada na Ushuru* |
| 1. | Aina zote za madini ya ujenzi | 12,000/= kwa tripu<br>150,000/= kwa muda wa miezi sita<br>300,000/= kwa muda wa mwaka mmoja |
| 2. | Kibali cha kuchimba madini ya ujenzi | 20,000/= kwa mwaka |
| 3. | Dust | 5000/= per cubic m3 |
| 4. | Kibali cha kufyatua tofali za udongo au kuchoma tanuru | 100,000/= kwa tanuru kwa mwaka. |

| II. ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI NA VIFAA VYA HALMASHAURI | | |
|---|---|---|
| *Na.* | *Aina ya kifaa* | *Kiwango cha ada na ushuru* |
| 1 | (i) Kumbi za Halmashauri.<br>(a)Ukumbi mkubwa<br>(b)Ukumbi mdogo | <br>(a)200,000/= kwa siku moja<br>(b) 50,000/= kwa siku moja |
| 2 | (ii) Viti vidogo<br>(iii) Viti vya chuma | ths. 300/=@ kimoja kwa siku<br>ths 500/= @ kimoja kwa siku |
| 3 | Meza ndogo | Ths 500/= @ kimoja kwa siku moja |
| 4 | Meza kubwa | Ths 1000/= @ kimoja kwa siku moja |
| 5 | Vibanda vya Halmashauri kuzungusha stendi kuu | Kwa mujibu wa mkataba |
| 6. | Vibanda vya biashara sokoni | Kwa mujibu wa mkataba |
| 7, | Majengo mengine ya Halmashauri | Kwa mujibu wa mkataba |

III. USHURU WA UKAGUZI WA NYAMA

| *Na.* | *Aina ya mfugo* | *Kiwango cha ada na ushuru* |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 4000/= |
| 2. | Mbuzi/ kondoo | 1000/= |
| 3. | Nguruwe | 2000/= |

IV.ADA YA UTUMIAJI MASOKO.

| | *Aina ya bidhaa* | *Kiwango cha ada na ushuru* |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa meza | Tsh. 500/=kwa siku |

| V. USHURU WA MIFUGO, MINADA, BIDHAA NA MAGULIO MENGINE | | |
|---|---|---|
| Na. | Aina ya Bidhaa | Kiwango cha ada na ushuru |
| 1 | Ng'ombe | 4,000/=@ng'ombe |
| 2 | Kondoo | 1000/=@kondoo |
| 3 | Mbuzi | 1000/=@mbuzi |
| 4 | bidhaa zinazotengenezwa viwandani/ karakana | 1000/= |
| 5 | Wauza mitumba | 1000/= |
| 6 | Wauza bia na vinywaji baridi | 1,000/= |
| 7 | Wauza nafaka | 1000/=@ gunia |
| 8 | Ndege(kuku,bata) | 1000/= |
| 9 | Pombe za asili | 1000/= |
| 10 | Wauza madawa ya asili | 1000/= |
| 11 | Wauza vipuri vya baiskeli,pikipiki,magari | 1000/= |
| 12 | Wauza dagaa | 1000/= |
| 13 | Wauza samaki | 1000/= |
| 14 | Wauza chumvi,nyama na mboga za majani | 1000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 15 | Wauza vyungu | 1000/= |
| 16 | Wauza vyombo vya nyumbani | 1000/= |
| 17 | Wauza viatu | 1000/= |
| 18 | Wauza nguo mpya | 1000/= |
| 19 | Mafundi baiskeli | 1000/= |
| 20 | Bidhaa nyingine ambazo hazijatajwa | 1000/= |
| 21 | Mifugo mingine ambayo haijatajwa | 1000/= |
| 22 | Mafundi baiskeli | 1000/= |
| 23 | Bidhaa nyingine ambazo hazijatajwa | 1000/= |
| 24 | Mifugo mingine ambayo haijatajwa | 1000/= |

| VI. ADA YA UKODISHAJI MITAMBO | | |
|---|---|---|
| Na. | Aina ya kifaa | Kiwango cha Ada na Ushuru kwa siku |
| 1. | 10 tons isuzu tipper | 2500/= Per Km |
| 2. | 7tons isuzu tipper | 150,000/= |
| 3. | 31/2 cargo truck with crane | 120,000/= |
| 4. | Concrete mixer | 80,000/= |
| 5. | Concrete poker vibator | 50,000/= |
| 6. | Air compressor | 200,000/= |
| 7. | Steel wheel roller | 250,000/= |
| 8. | Plate compactor | 70,000/= |
| 10 | Water bowser | 150,000/= |
| 11 | Bitumen boller with sprayer | 150,000/= |
| 12 | Hand pump bitumen sprayer | 60,000/= |
| 13 | Chipping spreader | 200,000/= |
| 14 | Wheel loader | 600,000/= |
| 15 | Motor grader | 1,000,000/= kwa masaa 8. |

| | | |
|---|---|---|
| 16 | Vifaa vya GPS | Kwa mujibu wa mkataba |

| | VII. VIBALI VYA UJENZI | |
|---|---|---|
| | *Aina ya ujenzi* | *Kiwango cha Ada na Ushuru* |
| 1. | Viwanja vyote vya makazi | 50,000/=<br><br>ujenzi wa nyumba zaidi ya moja @nyumba inayoongezeka italipiwa 20,000/= |
| | Makazi na Biashara | 100,000/= |
| 2. | Taasisi mbalimbali<br><br>(shule,vyuo, nyumba za ibada,ofisi mbalimbali, kumbi) ambazo sio ghorofa | 300,000/= |
| 3. | Viwanda vikubwa | 300,000/= |
| 4. | Viwanda vya uzalishaji | 150,000/= |
| 5. | Viwanda vidogo | 100,000/= |
| 6. | Vituo vya mafuta | 300,000/= |
| 7. | Ukarabati | 35,000/= |
| 8. | Uzio/fensi(a)Taasisi<br><br>(b)Binafsi | 1000 kwa mita moja ya mzunguko.<br><br>1000/=kwa mita moja ya mzunguko. |
| 9 | Hifadhi ndogo,uwanja wa michezo,hoteli za utalii ambazo sio ghorofa | 200,000/= |
| 10. | Ghorofa<br><br>-ghorofa 1-3 | 175,000/= |
| 11. | -ghorofa 4-6 | 200,000/= |
| 12. | -ghorofa 6 na kuendelea | 200,000/= na<br><br>75,000/= kwa kila ghorofa inayoongezeka |
| 13. | Kuhuisha (renew) kibali cha ujenzi wa ghorofa | 200,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 14. | Kusimika minara ya mawasiliano | 1,000,000/= |
| 15. | Kuhuisha (renew) kibali cha ujenzi usio ghorofa | Ada ni kama ilivyo kwa kibali cha awali |
| 16. | Minara iliyosimikwa Maeneo ya Watu binafsi | 10% ya pesa ya mkataba. |
| 17. | Ghala na Bohari | 250,000/= |
| 18 | Mabadiliko ya Matumizi ya Ardhi | 200,000/= |
| 19 | Sehemu za kuoshea Magari(Car Wash) | 100,000/= |
| 20 | Maeneo ya Mapumziko (recreational Centres) | 100,000/= |

VIII.ADA NA USHURU WA MAEGESHO YANAYOMILIKIWA NA HALMASHAURI.

| *Na* | *Aina ya gari* | *Kiwango cha ada na ushuru* |
|---|---|---|
| 1 | Gari chini ya tani 10 | 2500/= kwa siku |
| 2 | Lori zaidi ya tani 10 | 3000/= kwa siku |
| 3 | Gari dogo | 1000/= kwa siku |
| 4 | Pikipiki ya magurudumu mawili | 500/= kwa siku |
| 5 | Pikipiki ya magurudumu matatu | 500/= kwa siku |
| 6 | Pick up/station wagon | 1500/= kwa siku |
| 7 | Ada ya kutunza gari lililokamatwa au kuzuiliwa | 20,000 kwa siku |
| 8 | Ada ya kutunza pikipiki iliyokamatwa au kuzuiliwa | 10,000 kwa siku |
| 9 | Guta | 500/= |

| | IX. USHURU WA STENDI | |
|---|---|---|
| *Na.* | *Aina ya gari* | *Kiwango cha ada na ushuru* |
| 1 | Mabasi makubwa | 3000/= kwa siku |
| 2 | Mabasi ya kati | 2500/= kwa siku |
| 3 | Hiace | 2000/= kwa siku |

*Tangazo la Serikali Na. 670 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Magari madogo | 1000/= kwa siku |
| 6 | Magari ya mizigo<br>-tani 1-3<br>-tani 4-10 | <br>1000/= kwa siku<br>2500/= kwa siku |
| 7 | Pikipiki ya magurudumu matatu | 500/= kwa siku |
| 8 | Pikipiki ya magurudumu mawili | 300/= kwa siku |

X. USHURU WA HUDUMA ZA USAFI

| Na | Taasisi | Kiwango cha ada na ushuru kwa mwaka | Kiwango cha Ushuru kwa mwezi |
|---|---|---|---|
| 1 | Taasisi zote na mashirika | 360,000/= | 30,000/= |
| 2 | Wauza matunda | 60,000/= | 5000/= |
| 3 | Viwanda vikubwa | 600,000/= | 50,000/= |
| 4 | Viwanda vya kuoka mikate(bakery) | 360,000/= | 30,000/= |
| 5 | Hoteli za kitalii | 300,000/= | 25,000/= |
| 6 | Migahawa | 60,000/= | 5000/= |
| 7 | Useremala | 50,000/= | 4,200/= |
| 8 | Wauza mbao | 60,000/= | 5,000/= |
| 9 | Mashine ndogo za kusaga na kukoboa | 50,000/= | 2,500/= |
| 10 | Duka la jumla | 60,000/= | 5,000/= |
| 11 | Duka la rejareja | 25,200/= | 2,100/= |
| 12 | Ghala (“godown”). | 200,000/= | 15,000/= |
| 13 | Viwanda vidogo vya kukamua mafuta | 50,000/= | 5,000/= |
| 14 | Bucha za samaki au nyama | 30,000/= | 2,500/= |

*Tangazo la Serikali Na. 670 (Linaendelea.)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15 | Machinjio. | 300,000/= | 15,000/= |
| 16 | Baa na mgahawa. | 60,000/= | 5,000/= |
| 17 | Mini super market. | 50,000/= | 5,000/= |
| 18 | Vilabu vya pombe za kienyeji. | 30,000/= | 2,500/= |
| 19 | Nyumba za kuishi. | 12,000/= | 1,000/= |
| 20 | Saluni za wanaume na wanawake | 24,000/= | 2,500/= |
| 21 | Grocery (mini bar) | 30,000/= | 2,500/= |
| 22 | Nyumba za kulala wageni | 60,000/= | 5,000/= |
| 23 | Gereji | 40,000/= | 4000/= |
| 24 | Vituo vya mafuta | 50,000/= | 4,200/= |
| 25 | Maduka ya vifaa vya ujenzi na | 60,000/= | 5,000/= |
| 26 | Maduka ya nguo na viatu | 25,000/= | 2,500/= |
| 27 | Maduka ya dawa (pharmacy) | 50,000/= | 4,200/= |
| 28 | Maduka ya dawa muhimu | 25,000/= | 2,000/= |
| 29 | Maduka ya mikate na vitafunwa | 25,000/= | 2,000/= |
| 30 | Maduka ya vyombo | 25,000/= | 2,000/= |
| 31 | Maduka ya kuuza magodoro na samani | 25,000/= | 2,000/= |
| 32 | Maduka ya kuuza spea za magari, pikipiki na baiskeli | 50,000/= | 4,200/= |
| 33 | Maduka ya kuuza shajala na kurudufisha (photocopy) | 50,000/= | 4,200/= |
| 34 | Maduka ya kuuza vipodozi | 25,000/= | 2,000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 670 (Linaendelea.)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 35 | Maduka ya kuuza simu au saa. | 24,000/= | 2,000/= |
| 36 | Mama na baba lishe | 24,000/= | 2,000/= |
| 37 | Mgahawa | 60,000/= | 5,000/= |

XI. USHURU WA SOKO KWA MAZAO AU BIDHAA ZITOKANAZO NA MAZAO SOKONI

| *Na.* | *Aina ya Bidhaa* | *kiwango cha Ada na Ushuru* |
|---|---|---|
| 1 | Mahindi | 1000/=@gunia kwa mzigo zaidi ya tani moja |
| 2 | Maharage | 1500/=@gunia kwa mzigo zaidi ya tani moja |
| 3 | Muhogo | 500/=@ gunia kwa mzigo zaidi ya tani moja |
| 4 | Mtama | 1500/=@ gunia kwa mzigo zaidi ya tani moja |
| 5 | Mpunga | 1000/=@ gunia kwa mzigo zaidi ya tani moja. |
| 6 | Dagaa | 3% ya bei ya dagaa ya siku husika |
| 7 | Ushuru wa Samaki na Mazao ya Samaki | 3% ya bei ya samaki ya siku husika. |
| 8 | Vitunguu | 1500/=@gunia kwa mzigo zaidi ya tani moja |
| 9 | Alizeti | 1000/=@ gunia kwa mzigo zaidi ya tani moja |
| 10 | Kabeji, machungwa, miwa, nanasi,ndizi,parachichi | 7000/= kwa tani moja |
| 11 | Viazi | 1500/=@gunia kwa mzigo zaidi ya tani moja |
| 12 | Hoho | 500/= kwa tenga kwa mzigo zaidi ya tani moja |
| 13 | Karanga | 2500/= @gunia kwa mzigo zaidi ya tani moja |
| 14 | Njegere maganda | 1000/=@gunia kwa mzigo zaidi ya tani moja |

| | | |
|---|---|---|
| 15 | Pumba za mahindi | 500/=@gunia |
| 16 | Pumba za Mpunga | 500/=@gunia |
| 17 | Mashudu ya Alizeti | 1000/=@gunia |
| 18 | Nyanya | 500/=@tenga kwa mzigo zaidi ya tani ya moja |
| 19 | Mchele | 2000/= @ gunia kwa mzigo zaidi ya tani moja |
| 20 | Unga | 500/=@ gunia kwa mzigo zaidi ya tani moja |
| 21 | Bidhaaa nyingine ambazo hazijatajwa katika sehemu hili | 3,000/=@gunia kwa mzigo zaidi ya tani moja |

XII. ADA AU USHURU WA SHUGHULI ZA BURUDANI, UTAMADUNI, SANAA NA MATANGAZO

| NA | AINA YA HUDUMA | KIWANGO CHA ADA AU USHURU |
|---|---|---|
| 1 | Washereheshaji | 50,000/= kwa tukio |
| 2 | Wapambaji wa kumbi za burudani ( harusi, sherehe za jikoni, sherehe za kuaga binti na nyinginezo) | 30,000/= kwa tukio |
| 3 | Wamiliki wa kumbi mbalimbali | -ukumbi unaochukua watu 100-200 shilingi 50,000/=kwa siku<br><br>-ukumbi unaochukua watu 300-500 shilingi 100,000/= kwa siku |
| 4 | Matangazo ya barabarani ya sherehe | 40,000/= kwa tukio moja kwa<br><br>siku |
| 5 | Wapishi wa vyakula | 30,000/= kwa tukio moja kwa siku |
| 6 | Picha jongevu na mnato | 30,000/= kwa tukio moja kwa siku. |
| 7 | Matangazo ya kuuza bidhaa zinazopungua bei (promotion) | 40,000/= kwa tangazo |
| 8. | Maombi ya kibali cha kufanya Tiba za Jadi | 30,000/= kwa siku |
| 9 | Matamasha | 100,000/= kwa tamasha |

*Tangazo la Serikali Na. 670 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 10 | Fete na bahati nasibu | 20,000/= kwa siku |
| 11. | Mnada (a) mali isiyohamishika<br>(b)mali nyinginezo | 1% ya kuuzia.<br>40,000/= |
| 14 | Kupiga muziki ukumbi mkubwa | 50,000/= kwa siku |
| 15. | Kupiga muziki ukumbi mdogo | 30,000/= kwa siku |
| 16. | Matangazo ya Biashara kwa kutumia vipaza sauti; au vipeperushi; au vitambaa na; au fani za sanaa ambazo hazijatajwa hapo juu. | 30,000/= kwa siku. |
| 17. | Kumbi za video na mipira | -Ukumbi Mkubwa 200,000/=<br>-Ukumbi wa Kati 150,000/=<br>-Ukumbi Mdogo Mjini 100,000/=<br>-Ukumbi Mdogo Vijijini 50,000/= |
| 18 | Betting Machines (Slot Machines) | 300,000/= kwa Mwaka |

Ada zote katika sehemu ya XII (1) -(7) zitalipwa kwa pamoja na mwenye sherehe

XIII. ADA YA KULAZA MAGARI MAENEO YANAYOMILIKIWA NA HALMASHAURI

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Mabasi makubwa | 3000/= kwa siku |
| 2 | Mabasi madogo/hiace | 2000/= kwa siku |
| 3 | Gari ndogo | 1000/= kwa siku |
| 4 | Pick up au station wagon | 1500/= kwa siku |

XIV. ADA ZA UKATAJI BARABARA

| na | aina ya barabara | ukubwa | gharama |
|---|---|---|---|
| 1 | Barabara ya lami | mita moja | 200,000/= |
| 2 | Barabara ya changarawe | mita moja | 80,000/= |
| 3 | Barabara ya vumbi | mita moja | 30,000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 670 (Linaendelea.)*

XV. ADA ZA USAJILI WA TAXI BAJAJI

| na | aina ya gari | Ada | Muda |
|---|---|---|---|
| 1 | Taxi | 100,000/= | Mwaka mmoja |
| 2 | Bajaji | 100,000/= | Mwaka mmoja |

XVI. USHURU WA MAZAO YA KILIMO

| Na. | Aina ya Mazao | Kiwango |
|---|---|---|
| 1 | Mazao ya biashara. | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |
| 2. | Mazao ya chakula | Asilimia mbili (3%) ya bei ya kununulia. |

XVII. USHURU WA MAZAO YA MISITU

| *Na.* | *Aina ya Mazao* | *Kiwango cha Ushuru* |
|---|---|---|
| *1* | *Aina zote za mazao ya Misitu* | *Asilimia tano (5%) ya bei ya kununulia* |

XVIII.USHURU WA HUDUMA YA CHOO NA BAFU

| *Na.* | *Aina ya huduma* | *Kiwango cha Ushuru* |
|---|---|---|
| *1* | *Choo* | *300/=* |
| *2* | *Bafu* | *500/=* |

XIX.ADA YA USAJILI WA VIKUNDI VYA KIJAMII

| | | |
|---|---|---|
| | *Ada ya maombi ya usajili wa kikundi* | *20,000/=* |

XX.USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI

| | | |
|---|---|---|
| | *Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni* | *Asilimia 10 ya bei ya chumba kilicholaliwa na mteja* |

JEDWALI LA TATU

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 10)*

KUFIFILISHA KOSA

Mimi…………………………………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, kwamba mnamo tarehe ………mwezi………. Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema za mwaka 2020.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halamashauri ya Wilaya ya Sengerema, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe………………………………. ya Mwezi…………………. Mwaka…………………

Jina…………………………………………Saini………………………………………

Mbele ya:

Jina………………………………………...Cheo…………………………………….

Saini………………………………………Tarehe……………………………………

Nembo na Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizo kwa Azimio lililopitishwa na mkutano wa baraza la Madiwani uliopitishwa tarehe 3/12/2019 na ubandikaji huo kushuhudiwa na:-

MAGESA MAFURU BONIFACE,
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Wilaya*
*Sengerema*

YANGA EVARIST MAKAGA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya*
*Sengerema*

S.L

NAKUBALI

Dodoma
5 Agosti, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB),
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikoa na Serikali za*
*Mitaa*